# Unyambulishi wa Nomino na Vitenzi katika Kikahe

**Kulikoyela Kahigi**

**Ikisiri**

Makala hii inawakilisha uchambuzi wa awali wa unyambulishi wa nomino na vitenzi katika Kikahe, lugha ya Kibantu inayozungumzwa katika kata ya Kahe, Moshi Vijijini. Unyambulishi wa nomino unahusu uzalishaji wa nomino kutoka kwenye vitenzi, vivumishi na tarakimu, na unyambulishi wa vitenzi unahusu utendea, utendwa, utendeshi, utendeka, utendani na utenduzi. Uchambuzi huu wa unyambulishi unaonyesha kuwa Kikahe bado kimehifadhi michakato muhimu inayochukuliwa kuwa ilikuwemo katika Mama-Bantu, na ambayo bado i hai katika lugha nyingi za Kibantu. Hata hivyo, imeonekana kwamba michakato mingine imeshatoweka.

## 1.0 Utangulizi

Kikahe ni miongoni mwa lugha chache za Kibantu ambazo ziko hatarini kutoweka. Kwa mujibu wa uainishaji wa Guthrie (1948) lugha hii iko katika kundi la lugha za Kichaga; aliita E.30. Mradi wa Lugha za Tanzania (2008), katika utafiti wake wa wasemaji wa lugha za Tanzania, umekadiria kuwa Kikahe kinaongewa na watu wachache (takriban 9,035), ambao wanazidi kupungua kwa kadiri vizazi vinavyozidi kupokezana. Uchambuzi huu wa kipande cha sarufi cha Kikahe ni wa kwanza; na ni taarifa fupi itokanayo na utafiti unaoendelea kuhusu Kikahe. Lengo la utafiti mpana ni kuandika sarufi ya Kikahe, bali makala hii inahusu unyambulishi wa nomino na vitenzi. Unyambulishi wa aina nyingine za maneno (mathalani vivumishi) haujafanyiwa utafiti.

Unyambulishi, kama unavyojidhihirisha katika lugha za Kibantu na lugha nyingine, ni mchakato unaozalisha aina mpya za maneno au unaoongeza maana fulani kwenye mzizi/shina (taz. Katamba 1993). Kisarufi, unyambulishi husigana na uambatizi, mchakato wa kisarufi unaojumuisha kategoria kama za nafsi, njeo, hali, ngeli/jenda, nia na idadi. Utafiti mpana kuhusu sarufi ya Kikahe unazingatia uambatizi pia, lakini hatuugusii katika makala hii fupi.

Makala inahusu nomino zinazonyambulishwa kutokana na vitenzi, vivumishi na tarakimu, na unyambulishi wa vitenzi unaolenga maumbo ya utendea, utendeka, utendwa, utendeshi na utendani kulingana na data ambayo tunayo hivi sasa[1].

---

[1]Data iliyotumika hapa ilikusanywa katika utafiti uliofanyika Kahe mwishoni mwa 2004 na mwanzoni mwa 2005. Sehemu ya data hiyo imetumika katika kuandaa Kahigi (2008), taz. Utangulizi wa kitabu hicho.

## 2.0 Unyambulishi wa Nomino

Nomino katika Kikahe, kama zilivyo katika lugha nyingi duniani, ni za aina kuu mbili: zile zisizotokana na unyambulishi na zile zinazotokana na unyambulishi. Hapa tutaeleza michakato inayotumika kuzalisha nomino za aina ya pili. Michakato hii inajumuisha:

- Unyambulishi kutokana na vivumishi na tarakimu
- Unyambulishi kwa kubadili ngeli
- Unyambulishi kutokana na vitenzi

### 2.1Unyambulishi kutokana na vivumishi na tarakimu

Vivumishi na tarakimu huunda nomino katika ngeli ya 14, ambayo ni ngeli ya nomino dhahania. Nomino nyambulishi zinaundwa kwa kupachika kiambishi *u* kwenye mashina ya vivumishi na tarakimu, kama mifano ifuatayo inavyoonyesha:

| | | |
|---|---|---|
| *uradu* | ‘utatu’ | (<-*radu* ‘tatu’) |
| *unya* | ‘une’ | (<-*nya* ‘-ne’) |
| *uvicwa* | ‘ubaya’ | (<-*vicwa*‘baya’) |
| *uca* | ‘uzuri’ | (<-*ca* ‘zuri’) |
| *uvi* | ‘uwili’ | (<-*vi* ‘wili’ ) |
| *umu* | ‘umoja’ | (<-*mu* ‘moja’) |
| *udue* | ‘ukubwa’ | (<-*due*‘kubwa’) |
| *ufuhi* | ‘ufupi’ | (<-fuhi ‘fupi’) |

### 2.2 Unyambulishi kwa badiliko la ngeli

Unyambulishi wa namna hii hutokea pindi shina la nomino linapotumika na kiambishi-ngeli zaidi ya kimoja, kwa mfano:

***m**kahe* ‘mtu wa chimbuko la Kahe’ (Ngeli 1)
***u**kahe* ‘eneo la Kahe’ (Ngeli 14)
***ki**kahe* ‘lugha isemwayo na watu wa Kahe’ (Ngeli 7)

Ingawa maneno haya yanahusiana kwa kuwa na shina moja, *-kahe,* yanatofautiana kimaana; na tofauti hii inatokana na tofauti baina za viambishi. Nomino ya kwanza, mkahe, iko katika ngeli ya 1 (ngeli ya viumbe-watu); nomino ya pili, ukahe, iko katika ngeli ya 14, ambayo ni ngeli ijumuishayo nomino dhahania, nomino zinazorejelea nchi, na nyinginezo. Mfano wa tatu, kikahe, ni nomino iliyo katika ngeli ya 7, inayojumuisha vitu, lugha, n.k.

Hata hivyo, mifano yenye masafa mapana zaidi ya unyambulishi kwa badiliko la ngeli ni ile ihusuyo nomino kuwa nomino dogeshi, nomino kuzishi na nomino mahali.

#### 1.1.1 Nomino dogeshi

Hapa viambishi ngeli vya umoja ni viwili: *ki* na *ka*. Kiambishi ngeli cha wingi kwa vyote ni *shi.* Mifano ifuatayo inaonyesha hali hii:

| Nomino kutoka Ngeli ya 1 | | Wingi |
|---|---|---|
| *ka/kimndu/kimndu* | 'kijitu' | *shimndu* |
| *ka/kimndumka* | 'kanakake' | *shimnduvaka* |
| *ka/kimndumi/* | 'kanaume' | *shimnduvami* |

| Nomino kutoka Ngeli ya 3 | | |
|---|---|---|
| *ka/kikidi* | 'kijiti' | *shishidi* |
| *ka/kimwashi* | 'kimkia' | *shimwashi* |
| *ka/kindusu* | 'kijikamba' | *shindusu* |

*ki* inaweza pia kutumika kwa vitu vioevu kuonyesha 'kiasi kidogo':

| | |
|---|---|
| *kimringa* | 'maji kidogo' |
| *kicumbi* | 'chumvi kidogo' |
| *kiwari* | 'pombe kidogo' |

### 1.1.2 Nomino kuzishi

Katika umoja, nomino kuzishi huchukua kiambishi i na ji. Kiambishi i hutokea kabla ya mashina yanayoanza na konsonanti, na ji kabla ya mashina yanayoanza na irabu. Wingi wa nomino huundwa na kiambishi ma. Mifano ya nomino za namna hii ni:

**Kutoka ngeli ya 3:**

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| *imshi* | 'mchi' | *mamshi* |
| *imwashi* | 'mkia mkubwa' | *mamwashi* |
| *imsha* | 'mwiba mkubwa' | *mamsha* |

Kutoka ngeli ya 11:

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| *jiolumi* | 'ulimi mkubwa' | *malumi* |
| *jiohi* | 'kiganja kikubwa' | *maohi* |
| *jiolong'oi* | 'jogoo mkubwa' | *maolong'oi* |

### 1.1.3 Vimahali

Nomino zinageuka kuwa vimahali kwa kuambishwa kiambishi mahali– *nyi*; kiambishi hiki huambishwa kwenye nomino kamili, yenye muundo: kiambishi-tangulizi+shina la nomino, kama inavyoonyeshwa hapa chini:

**Kutoka ngeli ya 3/4:**
*mdonyi* 'kichwani' *midonyi* 'vichwani'

**Kutoka ngeli ya 5/6:**
*risonyi* 'jichoni' *mesonyi* 'machoni'

**Kutoka ngeli ya 7/8:**
*kindonyi* 'kwenye kitu' *shindonyi* 'kwenye vitu'

**Kutoka ngeli ya 9/10:**

*numbenyi* 'nyumbani'

Mchakato wa kugeuza nomino kuwa vimahali unazihusu pia nomino dogeshi na kuzishi. Mifano ni hii ifuatayo:

**Nomino dogeshi:**

*kanumbenyi* 'kijumbani' *shinumbenyi* 'vijumbani'

**Nomino kuzishi:**

*Ikudendenyi* 'guuni' *madendenyi* 'maguuni'

## 1.2 Nomino zitokanazo na Vitenzi

Nomino zinazonyambulishwa kutokana na vitenzi zinaonyesha ruwaza za kawaida zikutwazo katika lugha nyingine za Kibantu. Nomino zinaweza kuzalishwa kwa viambishi nominishi –o, -i, -e, -u; kiambishi-tendwa kikifuatwa na irabu ya mwisho (yaani *wa*) na shina la kitenzi.

### 2.3.1 Nomino zinazonyambuliwa kwa kiambishi –o

Nomino zinazozalishwa zina maana yajumla ya 'tokeo la tendo la kitenzi'. Mifano ni hii ifuatayo:

| Shina la Kitenzi | Maana | Nomino nyambuo | Maana |
|---|---|---|---|
| vavasha | 'panga' | ivavasho | 'mpango' |
| seka | 'cheka' | seko | 'cheko' |
| deda | 'sema' | dedo | 'zungumzo' |
| tengeta | 'zingira' | mtengeto | 'mviringo' |
| kusara | 'fikiri' | makusaro | 'fikira' |
| pindikya | 'funga fundo' | pindikyo | 'fundo' |
| kunda | 'penda' | ukundo | nyaitisyo |
| tisya | 'piga chafya' | nyaitisyo | nyaitisyo |
| reghya | 'andika' | reghyo | 'andiko' |
| regha | 'chora' | regho | 'mchoro' |

Ruwaza hii ni zalifu kwa kiasi kikubwa.

### 2.3.2 Nomino zinazoundwa kwa kiambishi-nominishi –i

Kiasi kikubwa cha nomino zinyazonyambuliwa kwa kiambishi kwa njia hii zina maana ya kawaida ya utendaji, yaani mtu anayehusika katika kitendo kinachotajwa na kitenzi. Mifano ni hii ifuatayo:

| Shina la Kitenzi | Maana | Nomino nyambuo | Maana |
|---|---|---|---|
| lemba | 'danganya' | mlembi | 'mdanganyifu' |
| shinja | 'chinja' | mshinji | 'mchinjaji' |
| dema | 'lima' | mdemi | 'mkulima' |
| -orokiwa | 'pendwa; pendezwa' | nyaoroki | 'mpendwa' |
| ghera | 'vua' | mgheri | 'mvuvi' |
| regha | 'chora' | mreghi | 'mchoraji' |
| kolong'a | 'totii' | mkolong'i | 'mkaidi' |

Nomino zinazoundwa na kiambishi nominishi hiki huingizwa katika ngeli ya 1.

### 2.3.3 Nomino zinazozalishwa kwa kiambishi –e

Nomino za namna hii ni chache; nazo huchukua viambishi nya- na m-; mifano ni hii ifuatayo:

| Shina la Kitenzi | Maana | Nomino nyambuo | Maana |
|---|---|---|---|
| *pa* | 'fa' | *nyapie* | 'mfu; marehemu' |
| *lua* | 'ugua' | *nyaluwe* | 'mgonjwa' |
| *dema* | 'lima' | *mdeme* | 'shamba' |
| *punga* | 'fuga wanyama' | *nyapungie* | 'mfugaji' |
| *dambuka* | 'tembea' | *mdamkye* | 'mtembezi' |

### 2.3.4 Nomino zinazoundwa kwa –u

Kundi hili la nomino lina uzalifu wa kiwango cha chini kabisa. Mifano iliyo katika data yetu ni hii ifuatayo:

| Shina la Kitenzi | Maana | Nomino nyambuo | Maana |
|---|---|---|---|
| *kolong'a* | 'totii' | *ukolong'u* | utovu wa utii' |
| *pa* | 'fa' | *kipu* | 'kifo' |

Inafaa tuseme kwamba kiambishi–*u* kinashabihiana na–*o* kwa vile viambishi vyote huzalisha nomino ambazo maana zake huashiria tokeo la kitendo kionyeshwacho na kitenzi.

### 2.3.5 Nomino zinazonyambulishwa kwa –w+a

**Mifano michache inaweza kuonyesha ruwaza hii ya nomino:**

| Shina la Kitenzi | Maana | Nomino nyambuo | Maana |
|---|---|---|---|
| *pa* | 'fa' | *mpiwa* | 'mfiwa' |
| *kunda* | 'penda' | *nyakundiwa* | 'mpendwa' |
| *tija* | 'acha' | *nyatiwa* | 'mwachwa' |
| *via* | 'ambia' | *nyaleviwa* | 'mwambiwa' |

### 2.3.6 Nomino zinazotokana na shina la kitenzi

Ruwaza hii ina uzalifu wa kutosha. Nomino zinazonyambulishwa hapa zinatokana ama na 'unyambulishi kapa' (shina la kitenzi bila kiambishi) au shina la kitenzi likiwa limetanguliwa na kiambishi cha nomino. Baadhi ya mifano ni:

| Shina la Kitenzi | Maana | Nomino nyambuo | Maana |
|---|---|---|---|
| *pa* | 'fa' | *kipa* | 'matanga rasmi' |
| *ndenga* | 'umiza' | *ndenga* | 'ajali' |
| *lora* | 'onyesha' | *nyakulora* | 'alama' |
| *talua* | 'jibu' | *talua* | 'jibu' |
| *raadika* | 'chefua' | *raadika* | 'kichefuchefu' |
| *sesa* | 'chesha; chekesha' | *isesa* | 'ucheshi' |
| *tighila* | 'chechemea' | *nyetighila* | 'kilema' |
| *dombana* | 'jamiiana' | *idombana* | 'tendo la kujamiiana' |
| *ting'a* | 'fundisha' | *ting'a* | 'mwalimu wa siri' |
| *fugha* | 'lia' | *fugha* | 'kilio' |
| *deda* | 'sema' | *nyededa* | 'msemaji' |

Katika mifano hii, unyambulishi-kapa unaonekana katika *talua, ndenga, raadika, ting'a, fugha,*na uzalishaji wa nomino unaotumia shina la kitenzi likitanguliwa na kiambishi unaonekana katika *pa/kipa, lora/nyalulora, dombana/idombana, deda/nyededa, sesa/isesa* na *tighila/nyetighila.*

## 3.0 Unyambulishi wa Vitenzi

Kikahe kina minyambuliko ya vitenzi yenye uzalifu wa hali ya juu, kwa mfano utendea na utendani, na mingine ambayo ina uzalifu wa kati, kama utendeshi. Viambishi husika havitofautiani na vile vilivyo katika lugha nyingine za Kibantu. Hata hivyo, tofauti na baadhi ya lugha za Kibantu, maumbo nyambuo katika Kikahe hayapambanuliwi na kanuni ya tangamano la irabu, ambayo kwayo irabu ya juu (*i* au *u*) hutangamana na irabu ya kati

ya mzizi wa kitenzi. Katika Kikahe, hakuna tangamano hilo; irabu inabaki kuwa *i*. Katika sehemu hii, tunaeleza maumbo nyambulishi ambayo bado hai katika lugha hii.

### 3.1 Unyambulishi wa Kutendea

Huu ni unyambulishi wenye uzalifu wa hali ya juu. Mifano ni hii ifuatayo:

| Shina la Kitenzi | Maana | Umbo la Kutendea | Maana |
|---|---|---|---|
| *nya* | 'nya' | *nyia* | 'nyea' |
| *nywa* | 'nywa' | *nywia* | 'nywea' |
| *tema* | 'tema; kata' | *temia* | 'temea; katia' |
| *dika* | 'chukua' | *dikia* | 'chukulia' |
| *seka* | 'cheka' | *sekia* | 'chekea' |
| *suma* | 'chimba' | *sumia* | 'chimbia' |
| *toca* | 'choma | *tocia* | 'chomea' |
| *regha* | 'chora' | *reghia* | 'chorea' |
| *daha* | 'chota' | *dahia* | 'chotea' |
| *shishina* | 'chuja' | *shishinia* | 'chujia' |
| *sanja* | 'fua' | *sanjia* | 'fulia' |
| *ting'a* | 'fundisha' | *ting'ia* | 'fundishia' |

Umbo la kutendea huweza kutokea huku likifuatwa na umbo la kutendana, k.m. *nyiana* 'nyeana', *nywiana* 'nyweana', *temiana* 'temeana; katiana', n.k.

### 3.2 Unyambulishi wa kutendwa

Umbo la unyambulishi huu ni –w-. Unyambulishi huu ni miongoni mwa michakato yenye uzalifu wa kiwango cha juu. Mifano ni hii ifuatayo:

| Shina la Kitenzi | Maana | Umbo la Kutendwa | Maana |
|---|---|---|---|
| *laca* | 'geuza' | *lacwa* | 'geuzwa' |
| *dika* | 'chukua' | *dikwa* | 'chukuliwa' |
| *bara* | 'pasua' | *barwa* | 'pasuliwa' |
| *suma* | 'chimba' | *sumwa* | 'chimbwa' |
| *shinja* | 'chinja' | *shinjwa* | 'chinjwa' |
| *toca* | 'choma' | *tocwa* | 'chomwa' |
| *baca* | 'chonga' | *bacwa* | 'chongwa' |
| *regha* | 'chora' | *reghwa* | 'chorwa' |
| *shishina* | 'chuja' | *shishinwa* | 'chujwa' |
| *sanja* | 'fua' | *sanjwa* | 'fuliwa' |
| *ting'a* | 'fundisha' | *ting'wa* | 'fundishwa' |
| *nga* | 'pa' | *ngiwa* | 'pewa' |
| *kunda* | 'penda' | *kundwa* | 'pendwa' |

## 3.3 Unyambulishi wa Kutendeka

Ingawa utokeaji wake si mpana kama ulivyo ule wa kutendea na wa kutendwa, bali unyambulishi huu una uzalifu wa kutosha. Ifuatayo ni mifano:

| Shina la Kitenzi | Maana | Umbo la kutendeka | Maana |
|---|---|---|---|
| *tema* | 'tema; kata' | *temika* | 'temeka; katika' |
| *laca* | 'geuza' | *lacika* | 'geuka; geuzika' |
| *bara* | 'pasua' | *barika* | 'pasuka' |
| *suma* | 'chimba' | *sumika* | 'chimbika' |
| *shinja* | 'chinja' | *shinjika* | 'chinjika' |
| *toca* | 'choma' | *tocika* | 'chomeka' |
| *baca* | 'chonga' | *bacika* | 'chongeka' |
| *regha* | 'chora' | *regheka* | 'choreka' |
| *shishina* | 'chuja' | *shishinika* | 'chujika' |
| *sanja* | 'fua' | *sanjika* | 'fulika' |
| *ting'a* | 'fundisha' | *ting'ika* | 'fundishika' |
| *rughua* | 'fungua' | *rughuka* | 'funguka' |

Mifano hii inaonyesha kuwa umbo la kutendeka ni–*ik*- kwa mizizi ya vitenzi inayoishia na konsonanti (k.m. *ting'ika)* na –*k*- kwa mizizi inayoishia na irabu (k.m. *rughuka*).

## 3.4 Umbo tendeshi

Mifano ifuatayo inaonyesha kuwa kiambishi hiki kina alomofu mbili: -*ish*- na –*s*-:

| Shina la Kitenzi | Maana | Umbo tendeshi | Maana |
|---|---|---|---|
| *pa* | 'fa' | *pisha* | 'fisha' |
| *dema* | 'tema/kata' | *temisha* | 'temesha/katisha' |
| *laca* | 'badili' | *lacisha* | 'fanya kubadili' |
| *shina* | 'cheza' | *shinisha* | 'chezesha' |
| *kangarika* | 'stuka' | *kangarisa* | 'stusha' |

| | | | |
|---|---|---|---|
| *bingirika* | 'vingirika' | *bingirisa* | 'vingirisha' |
| *seka* | 'cheka' | *sesa* | 'chesha/chekesha' |
| *valuka* | 'geuka' | *valusa* | 'geuza' |
| *burua* | 'buruta' | *burusa* | 'burutisha' |

Umbo-tendeshi linaweza kufutatwa na umbo-tendwa na umbo-tendana, kama mifano ifuatayo inavyoonyesha: *demishwa* 'badilishwa', *shinishwa* 'chezeshwa', *seswa* 'chekeshwa', n.k.. na *demishana* 'limishana', *shinishana* 'chezeshana', *sesana* 'chekeshana', n.k.

### 3.5 Unyambulishi wa Kutendana

Unyambulishi huu waonekana kuwa hai kabisa katika lugha hii. Vitenzi 50 vilijaribiwa kwa wasemaji wa lugha hii kuhusiana na unyambulishi huu, na vyote viliuruhusu unyambulishi huu. Hapa tutatoa mifano michache:

| Shina la Kitenzi | Maana | Umbo tendani | Maana |
|---|---|---|---|
| *laca* | 'geuza' | *lacana* | 'geuzana' |
| *dika* | 'chukua' | *dikana* | 'chukuana' |
| *bara* | 'pasua' | *barana* | 'pasuana' |
| *seka* | 'cheka' | *sekana* | 'chekana' |
| *suma* | 'chimba' | *sumana* | 'chimbana' |
| *shinja* | 'chinja' | *shinjana* | 'chinjana' |
| *toca* | 'choma' | *tocana* | 'chomana' |
| *baca* | 'chonga' | *bacana* | 'chongana' |
| *regha* | 'chora' | *reghana* | 'chorana' |
| *shishinia* | 'chujia' | *shishiniana* | 'chujiana' |
| *sanjia* | 'fulia' | *sanjiana* | 'fuliana' |
| *ting'a* | 'fundisha' | *ting'ana* | 'fundishana' |

kama tulivyokwisha sema hapo juu, umbo-tendana linaweza kutanguliwa na umbo-tendea, mathalani *shishiniana* hapo juu, au linaweza kufuata umbo-tendeshi.

## 4.0 Hitimisho

Katika makala hii fupi tumeeleza kwa ufupi unyambulishi wa nomino na vitenzi katika Kikahe. Ni wazi kwamba utafiti zaidi unahitajika, si kuhusiana na unyambulishi huu tu, bali hata unyambulishi wa aina nyingine ambao unaweza kuwa hai au si hai tena. Mathalani michakato ifuatayo haijachunguzwa:

- Unyambulishi wa utenduzi: Katika data tuliyo nayo, tumegundua mfano mmoja tu wa utenduzi, punga 'funga' pungua 'fungua'. Inawezekana data pana zaidi inaweza kuonyesha mifano zaidi ya utenduzi.
- Uundaji wa vitenzi kutokana na nomino: Katika data tuliyo nayo kuna mfano mmoja tu wa mchakato huu, sonu 'aibu' → -sonusha 'aibisha'.

Inawezekana data pana zaidi inaweza kuonyesha mifano zaidi ya mchakato huu.

- Uundaji wa vitenzi kutokana na vivumishi: Mchakato huu unapatikana katika lugha nyingi za Kibantu, mathalani Kinyamwezi (Maganga na Schadeberg, 1992), Kisumbwa (Kahigi, 2008), Kinyambo (Rugemalira, 2005), n.k. Data ya Kikahe tuliyo nayo haionyeshi mchakato huu; huenda data pana zaidi ikaonyesha mchakato huu.

Kadhalika, inafaa kufanya uchunguzi zaidi kuhusu utokeaji wa viambishi dogeshi viwili – *ka-* na *ki-*. Vinatofautianaje? Je, ni tofauti ya kilahaja au ni ya kimaana?

Mwisho, tulinganishapo viambishi-nyambulishi vya Mama-Bantu vilivyoundilizwa na wanaisimu wa lugha za Kibantu (taz. Meeussen (1967) na Guthrie (1971, Juzuu 2:144)) na vile vitokeavyo katika Kikahe tunaona kuwa vile vya Kikahe vimepungua. Viambishi-nyambulishi kama *–agul-/-aguk-, -aguzi-, -ilizi-, -h-, -hal-, -am-, -al-, -at-* na *-uk-* (taz. Kahigi 2008:53-81) havionekani kamwe katika data tuliyo nayo. Ingawa utafiti unaendelea, lakini dalili zinaonyesha kuwa vimeshapotea.

Ni wazi kwamba masuala haya yote yanahitaji kutafitiwa zaidi, na utafiti wetu katika siku za usoni utajitahidi kuyashughulikia.

## Marejeleo


Guthrie, M. (1948) *The Classification of the Bantu Languages.* London: OUP.

Guthrie, M. (1967-71) *Comparative Bantu.* Juzuu 4. Farnborough: Gregg Press.

Kahigi, K. (2008) *Msamiati wa Kikahe-Kiingereza-Kiswahili.* LOT PUBLICATIONS: Lexicon Series. Dar es Salaam: Mradi wa Lugha za Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kahigi, K.K (2008) 'Derivation in Sisumbwa', katika *LOT PUBLICATIONS: Occasional Papers in Linguistics Series No. 3.* Dar es Salaam:Mradi wa Lugha za Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Maganga, C. and T.C. Schadeberg (1992) *Kinyamwezi.: Grammar, Texts, Vocabulary.* Rudiger Koppe Verlag. Koln.

Meeussen, A.E. (1967) 'Bantu Grammatical Reconstructions'. In AFRICANA LINGUISTICA III, 79-121.

Mradi wa Lugha za Tanzania (2008) *Atlasi ya Lugha za Tanzania.* Dar es Salaam: Machapisho ya Mradi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Rugemalira, J. (2005) 'A Grammatical Sketch of Runyambo'. In: LOT Publications. *Ocassional Papers in Linguistics Series,* No. 1:38-74. UDSM.

Schadeberg, T.C. (2003) Derivation. In: Nurse, D. and G. Philippson

*Series.* No. 1: 38-74. 2003. *The Bantu Languages,* kur.: 71-89. London and N.Y.: Routledge.